## Maswali

1. Yoshua alikutana na nani karibu na Yeriko?
2. Malaika aliambia Yoshua nini?
3. Waisraeli walifanya nini kwa siku 6?
4. Walizunguka kuta za mji wa Yeriko namna gani?
5. Siku ya saba walizunguka kuta za Yeriko mara ngapi?
6. Watu walifanya nini baada ya kutembea wakizunguka mara ya saba?
7. Nini ilifanyika Waisraeli walipopika kelele?
8. Wanajeshi wa Israeli walifanya nini?
9. Wapelelezi wawili walifanya nini?
10. Waisraeli walifanya nini walipopiga na kushinda Yeriko?

## Majibu

1. Yoshua alikutana na malaika –Nahodha wa jeshi la Mungu.
2. Mungu atasaidia Waisraeli kushinda Yeriko. Malaika alipea Yoshua maagizo ya Mungu.
3. Waisraeli walizunguka ukuta wa Yeriko mara moja kila siku kwa siku 6.
4. Kwanza wanajeshi, halafu makuhani 7 wakipiga tarumbeta za pembe za kondoo waume, halafu Sanduku, mwishowe watu wote wa Waisraeli. Wakitembea wakiwa kimya.
5. Siku ya saba Waisraeli walizunguka mara 7.
6. Waisraeli walipomaliza kuzunguka, walipiga kelele kwa sauti kuu.
7. Kuta za Yeriko zilianguka chini.
8. Wanajeshi waliingia Yeriko, wakaaribu kila kitu na kuichoma.
9. Wapelelezi wawili walienda kuchukuwa Rahabu. Waliokoa Rahabu na jamii yake.
10. Waisraeli walimhimidi na kumshukuru Mungu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 29 Yoshua na vita vya Yeriko

**Kwa Biblia** Yoshua mlango wa 5:13-15 na mlango wa 6

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima kila wakati tuheshimu Mungu kabisa. Mungu ni wa nguvu kuliko jeshi lolote. Mungu anasaidia watu wake wakimwamini

### Somo

Mji wa Yeriko ulikuwa wa nguvu. Pengine ulikuwa ndio mji wa nguvu zaidi kwa nchi ya Kanaani. Mji huu ulikuwa na kuta nzito na minara ya nguvu. Itakuwa vigumu kushinda Yeriko. Lakini Yoshua aliamini Mungu. Alijua Mungu atamsaidia.

Yoshua alikuwa kiongozi wa hekima. Alienda kuchunguza Yeriko kabla afanye mpango wa kuishambulia. Yoshua alipata kwamba mji ulifungiwa. Watu wa Yeriko waliogopa sana walipoona vile Waisraeli walivuka Mto wa Yordani. Watu wa Yeriko walifunga milango ya mji. Hakuna aliyekubaliwa kutoka wala kuingia.

Yoshua alitembea kando kando ya kuta kubwa ya Yeriko. Yoshua alijua kwamba Waisraeli wenyewe hawana nguvu ya kutosha kupigana na kushinda huo mji. Bunde tu Yoshua akakutana na mtu ameshika upanga mkononi. Yoshua alimuuliza, “Wewe ni rafiki au adui.” Alimjibu, “Hapana. Mimi ni nahodha wa jeshi la Bwana Mungu.” Yoshua aliinama chini na kusema, “Mungu ananiamrisha nifanye nini?”

Malaika alimwambia kwamba Mungu atasaidia Waisraeli washinde Yeriko. Malaika alimwambia chenye lazima wafanye na wafanye kikamilivu. Yoshua alirudi kambini. Aliambia Waisraeli kwamba Mungu ametuma malaika kusema chenye wanatakiwa wafanye. Waisraeli walifurahi sana waliposikia kwamba Mungu atawasaidia washinde Yeriko.

Mungu alisema kwamba lazima Waisraeli wazunguke Yeriko mara moja kila siku kwa siku sita. Watu wa silaha wataenda kwanza. Watafwatwa na makuhani saba wakipiga tarumbeta iliyotengenezwa kutoka kwa pempe za kondoo waume. Nyuma yao ilikuwa Sanduku na mwisho ni Waisraeli wote. Mungu alisema lazima kusikuwe na kelele. Mtu yeyote asizungumze wakati wanazunguka mji wa Yeriko. Kelele yoyote iwe ya makuhani wakipuliza pembe za kondoo. Mungu aliwambia, siku ya saba kila mtu atazunguka mji mara saba. Halafu wote watapasa sauti ya juu.



*Tarumbeta za pembe za kondoo waume*

Kwa siku sita, Waisraeli waliamka mapema. Walienda kwa mji wa Yeriko. Walitembea wakazunguka mji mara moja halafu walirudi kambini. Watu wa silaha walienda kwanza. Nyuma yao walikuwa makuhani saba wakitembea wamevaa majoho meupe. Walikuwa wanapiga tarumbeta za pembe za kondoo waume. Katikati ya mwandamano huo kulikuwa na Sanduku, na mwisho kabisa, Waisraeli wote. Walitembea wote wakiwa kimya.

Watu wa Yeriko waliona Waisraeli wakiwakujia mjini. Wakasanyika kwa kuta ili wawaone. Walitarajia Waisraeli wawashambulie. Lakini Waisraeli walitembea, wakazunguka mji na kwenda. Waisraeli walirudi wakizunguka kila asubuhi kwa siku sita.

Watu wa Yeriko walishangaa wakawa na wasi wasi. Mbona Waisraeli wanazunguka mji? Mbona wanatembea wakiwa kimya? Mbona Sanduku liko katikati ya mwandamano? Watashambulia mji lini? Waisraeli walikuwa wanafanya nini? Watu wa Yeriko waliogopa.

Siku ya saba Waisraeli waliamka asubuhi na kuenda Yeriko. Siku hiyo Mungu alikuwa amewambia watembee nawazunguka mji mara saba. Waisraeli walikuwa kimya walipotembea wakizunguka mji. Makuhani walipuliza pembe za kondoo. Makuhani walibeba Sanduku kwa utaratibu. Sanduku lilikuwa la maana sana. Ilikuwa ishara ya kuonyesha kwamba Mungu alikuwa nao kuwasaidia.

Labda watu waliokuwa kwa ukuta wa Yeriko walipigia Waisraeli kelele. Hata labda waliwatupia mawe. Lakini Waisraeli walinyamaza na kutembea wakizunguka ukuta. Waisraeli walitii Mungu kwa ukamilivu. Waliamini kwamba Mungu atawasaidia kushinda huo mji.

Waisraeli walisimama walipomaliza kuzunguka mara ya saba. Walikuwa wamezingira ukuta wa Yeriko wote. Makuhani walipiga tarumbeta ya pembe za kondoo waume mara ya mwisho kwa sauti ya juu. Yoshua aliambia watu, “Piga kelele; kwa maana Mungu amewapa huu mji.” Halafu watu wote wakapiga kelele kwa sauti za uwezo wao. Ukuta wa Yeriko ulianguka chini kwa kishindo kubwa. Kulikuwa na kelele kubwa na mahangaiko. Wanajeshi wa Waisraeli walikimbia juu ya vifusi vya kuta vilivyo lundikana. Walikimbia mpaka mjini. Bunde tu , Yeriko ilishambuliwa na kila kitu kiliharibiwa. Waisraeli walichoma Yeriko. Yeriko ilipokuwa ikiungua, Waisraeli walimhimidi Mungu. Mungu alikuwa amewasaidia kushinda adui wao.

Yoshua aliambia wapelelezi wawili walioenda Yeriko, “Enda muokoe Rahabu vile mlimwahidi.” Wale wapelelezi wakapata hiyo kamba nyekundu kwa dirisha la Rahabu. Walitoa Rahabu na jamii yake kutoka Yeriko. Rahabu na jamii yake walikaa na Waisraeli. Waliokolewa kutoka Yeriko kwa sababu waliamini Mungu na wakaokoa wapelelezi.

Usiku huo Waisraeli walifurahi. Walimhimidi Mungu kwa sababu uzuri na huruma yake. Mungu aliwapa ushidi kwa adui wao. Alikuwa amewasaidia kupiga na kushida mji mkubwa ya Yeriko.